JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

612

URAIA

Muda: Saa 3 **Alhamisi, 10 Mei 2018 asubuhi**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

1 810611 100018

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Orodhesha kazi nne za Mahakama Kuu ya Tanzania.

2. Taja misingi minne ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia.

3. Kwa kifupi elezea umuhimu wa kutumia kiongozi cha mwalimu katika ufundishaji wa somo la Uraia. Toa hoja nne.

4. (a) Kwa kifupi eleza maana ya maadili.

   (b) Ainisha mbinu tatu za kurekebisha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

5. Orodhesha faida nne za kutunza zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.

6. Katika hoja nne, onesha faida za mipango katika uchumi.

7. Elezea maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika andalio la somo la Uraia:
   (a) Ujuzi Mpya. (b) Tafakuri.

8. Bainisha stadi nne muhimu zinazohitajika kwa mtu kuwa raia mwema wa Tanzania.

9. Kwa kifupi chambua zana mbili za upimaji katika somo la Uraia.

10. (a) Nini maana ya tathmini?

    (b) Ainisha faida tatu za kumtathmini mwanafunzi katika somo la Uraia.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

11. Chambua shughuli tano za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

12. Katika hoja sita, eleza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu.

13. Eleza misingi mitatu ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania na katika hoja tatu, onesha namna mwananchi anavyofaidika na sera hiyo.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

14. Katika hoja sita, onesha athari za kutofundisha vyema mada ya uchambuzi wa masuala chanya na hasi ya kiserikali na kisiasa.

15. Chambua mbinu sita zinazoweza kutumika katika kukusanya machapisho bora ya ziada ya somo la Uraia.

16. Eleza umuhimu wa mwalimu wa somo la Uraia kufanya majaribio ya zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuzitumia. Toa hoja sita.